
**KITUO CHA MAENDELEO YA KILIMO MOGABIRI**

# USTAHIMILIVU DHIDI YA MABADILIKO YA TABIANCHI KWA WAKULIMA TARIME WAONGEZEKA

Katika kukabiliana na changamoto za mabadiliko ya tabianchi zinazolikumba eneo la Tarime, Kituo cha Kilimo Mogabiri (MFEC) kimeendelea kuwa mwanga wa matumaini kwa jamii za wakulima. Kupitia mafunzo ya kilimo hai, matumizi ya mbegu za asili, uhifadhi wa maji, upandaji miti, na matumizi ya taarifa za hali ya hewa, kituo hiki kimeongeza uwezo wa wakulima wa vijiji kama Kitenga, Nkerege, Kwisarara na Turugeti kufanya maamuzi sahihi ya kilimo na kuongeza uzalishaji katika mazingira yanayobadilika.

Mbali na hilo, MFEC imekuwa mstari wa mbele kusaidia familia za wakulima kujiongezea kipato kupitia miradi ya lishe mashuleni, uanzishwaji wa vikundi vya akiba na mikopo (VICOBA), na uhamasishaji wa matumizi ya mbinu rafiki kwa mazingira. Kwa ushirikiano wa karibu na jamii, shule, na viongozi wa vijiji, kituo hiki kimeweza kuleta mabadiliko chanya katika maisha ya watu wa Tarime – kiuchumi, kijamii na kimazingira.

Newsletter hii inakuletea baadhi ya mafanikio hayo, simulizi halisi na sauti za wanufaika walioguswa moja kwa moja na kazi hii muhimu.



## YALIYOMO


Mbegu za Asili, Urithi Wetu ........................2

Vitalu vya miti vyachochea harakati za mabadiliko ya tabianchi........................2

Tumaini Jipya wilayani Tarime ......................3

Kutana na Denis Chacha.......................3

Wakulima wanufaika na mafunzo ya kudhibiti wagonjwa katika mifugo na Mazao .................4

Kituo cha Kilimo chatoa msaada katika shule...5

## MBEGU ZA ASILI, URITHI WETU: MBEGU ZA ASILI ZA WALETEA WAKULIMA WA TARIME TUMAINI MPYA DHIDI YA MABADILIKO YA TABIANCHI.



Na: John Qambaro

Katika kukabiliana na changamoto zinazoletwa na mabadiliko ya hali ya hewa, wakulima wilayani Tarime hasa katika Kijiji cha Kewamamba wameendelea kuona thamani ya kurejea kwenye mbegu za asili. Kupitia mafunzo na uhamasishaji uliofanywa na Kituo cha Kilimo Mogabiri (MFEC) kwa kushirikiana na serikali za vijiji, wakulima wameanza kuhifadhi, kubadilishana, na kupanda mbegu za kienyeji zenye uwezo mkubwa wa kustahimili ukame na magonjwa. Pia Kijiji kimepiga hatua zaidi kwa kuanzisha benki ya Mbegu hizi za Asili kwa ajili ya kuzitunza na kuweza pia kubadilishana.

Bw. Nuhu Keraryo, Mkulima Kinara wa mbegu za Asili kutoka kijiji cha Kewamamba, anasema, “zamani tulitegemea mbegu tunazonunua kila mwaka, lakini hazikuwa na uhakika wa kustawi. Tangu nimeanza kutumia mbegu za asili nilizopata kupitia wadau mbalimbali, mavuno yangu yameongezeka na nina chakula cha kutosha na kwa sasa nimeinuka kiuchumi sana.”

Mbegu hizi si tu zinaendana na mazingira ya katika Vijiji vya Wilaya ya Tarime, bali pia hazihitaji matumizi makubwa ya pembejeo, jambo linalopunguza gharama kwa wakulima wadogo. Aidha, baadhi ya vikundi vya wakulima sasa vimeanza kuaanzisha mabenki ya mbegu na kufanya kubadilishano ya mbegu kama sehemu ya mikakati ya kujitegemea na kuongeza mnepo wa jamii zao dhidi ya mabadiliko ya tabianchi.

Kwa kutumia mbegu za asili, wakulima wanarejesha maarifa ya jadi na kujenga mustakabali endelevu wa kilimo unaozingatia mazingira na urithi wa kijamii.

*“Zamani tulitegemea mbegu tunazonunua kila mwaka, lakini hazikuwa na uhakika wa kustawi. Tangu nimeanza kutumia mbegu za asili nilizopata kupitia wadau mbalimbali, mavuno yangu yameongezeka na nina chakula cha kutosha na kwa sasa nimeinuka kiuchumi sana.” Nuhu*

## UPANDAJI MITI YACHOCHEA HARAKATI ZA KUKABILIANA NA MABADILIKO YA TABIANCHI TARIME

**Na. John Qambaro**

Wakulima na wanajamii katika vijiji 5 (Surubu, Kitenga, Turugeti, Kembwi na Nkerege) Tarime wamechukua hatua madhubuti za kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi kupitia uanzishaji wa vitalu vya miti na kampeni za upandaji miti. Hatua hii imekuwa ni njia endelevu ya kuhifadhi mazingira, kuzuia mmomonyoko wa udongo, na kurejesha uoto wa asili katika maeneo yaliyoathiriwa.




Kwa kushirikiana na viongozi wa vijiji, shule na vikundi vya wakulima, vimefanikiwa kuandaa vitalu vya miti ambapo miche ya aina mbalimbali kama Grevelia, Seregena, miti ya matunda na miti rafiki kwa mazingira imezalishwa. Miche hiyo husambazwa kwaajili ya kupandwa mashambani, pembezoni mwa makazi na vyanzo vya maji

Mbali na faida za kiikolojia, baadhi ya miti inayopandwa pia inatoa mazao ya kiuchumi kama matunda au kuni mbadala, hivyo kuwaongezea wananchi kipato. Upandaji wa miti umekuwa ni sehemu ya mikakati ya kijamii ya kuhimili athari za ukame, kupungua kwa rutuba ya udongo, na kuboresha maisha ya wakazi.

Kwa juhudi hizi, jamii ya Tarime inaendelea kujijengea uimara wa kukabiliana na changamoto za kimazingira kwa kutumia suluhisho rahisi, shirikishi na endelevu.

***“Kupitia kikundi chetu, tumezalisha miche zaidi ya 730. Tumepanda miti kuzunguka mashamba yetu ili kusaidia kivuli kwa mazao na kupunguza kasi ya upepo mkali na kwa ajili ya mbao.” Bw. Kenedy Nondi***



*Picha: Uwasilishaji wa Mpango kazi wa Kijiji Nkerege, katika Kukabiliana na athari za Mabadiliko ya tabianchi.*

## TUMAINI JIPYA KWA WAKULIMA TARIME

**Na. John Qambaro**

Katika wilaya ya Tarime, Kaskazini mwa Tanzania, jamii zimekuwa zikikabiliana na changamoto nyingi kutokana na mabadiliko ya tabianchi. Mabadiliko haya yameathiri mashamba yao, maeneo ya malisho ya mifugo na vyanzo vya maji. Eneo limekumbwa na mmomonyoko wa udongo ambao umeharibu miundombinu na mashamba. Changamoto kubwa zaidi imekuwa ukosefu wa maarifa sahihi ya jinsi ya kukabiliana na athari hizi. Watu wa Tarime walihisi kusahaulika sauti zao hazikusikilizwa, na maarifa yao ya asili hayakutumiwa ipasavyo katika kutafuta suluhisho. Hata hivyo, pamoja na yote hayo, wananchi wa Tarime wameendelea kuonyesha uimara na uthubutu katika kukabiliana na hali hii kwa kutumia njia bunifu na kushirikiana kujenga maisha bora.

Kituo cha Kilimo cha Mogabiri kimekuwa kama taa ya matumaini katika mazingira haya yenye changamoto. Kimeona umuhimu wa kushirikisha jamii kwa karibu ili kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi. Kupitia mbinu ya **Participatory Assessment of Climate and Disaster Risks (PACDR),** Kituo cha Kilimo Mogabiri kimeleta mabadiliko makubwa Tarime. Mbinu hii inatambua maarifa ya ndani ya jamii na kuwahamasisha wanajamii kushiriki moja kwa moja katika kutathmini hali ya hewa, kubaini hatari zinazotokana na mabadiliko ya tabianchi, kuweka vipaumbele vya hatari hizo na kupanga mikakati ya kupunguza madhara. Kwa njia hii, jamii zimeanza kuwa sehemu ya suluhisho, si waathirika tu wa mabadiliko haya.

Gibe Marwa, mkazi wa kijiji cha Nkerege, alisema, ***"Tumeweza kutambua athari mbalimbali za mabadiliko ya tabianchi na kushirikiana kupanga mikakati ya kukabiliana nazo."***

Nguvu hii mpya ya kujitambua na kushiriki kupambana na changamoto za tabianchi imekuwa mabadiliko makubwa kwa wakazi wa kijiji chao.

Sasa, watu wa Tarime waliodumu na changamoto, hasa wa vijiji vya Nkerege, Kitenga Turugeti na Kwisarara, wameweza kutumia maarifa waliyopata na ushiriki wa jamii kukabiliana na hatari za mabadiliko ya tabianchi. Wameanza kutumia mbinu mpya kama kulima mazao yanayostahimili ukame na kutumia mbegu bora. Pia wanatumia mbinu rafiki kwa mazingira katika kilimo.

Jamii hizi zimeanza kupanda miti maeneo yaliyoharibika na kufanya maamuzi sahihi shambani kwa kutumia taarifa za hali ya hewa na tabianchi. Mabadiliko haya yanaonesha jinsi suluhisho linaloongozwa na jamii linavyoweza kuwa na nguvu katika kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi.

## KUTANA NA DENIS CHACHA

Tumekuwa tukikumbana na changamoto mbalimbali katika shughuli za kilimo kwa misimu tofauti kutokana na kutotabirika kwa msimu wa mvua na changamoto ya kutopata mazao ya kutosha majumbani mwetu, kutokana na ukweli kwamba shughuli kuu ya kila kaya ni kilimo. Pia, tumekuwa tukiziona changamoto hizi kama jambo la kawaida bila kujua kuwa ni tatizo kubwa katika shughuli zetu za kilimo, anasema Denis Chacha (52), mmoja wa wakulima walioolengwa na mradi kutoka kikundi cha Taitakya katika kijiji cha Kitenga, wilaya ya Tarime, mkoa wa Mara.

Anasema kuwa, baada ya kupatiwa mafunzo mbalimbali kutoka Kituo cha Maendeleo ya Kilimo Mogabiri (Mogabiri Farm Extension Centre), hasa juu ya matumizi ya taarifa za hali ya hewa, jinsi ya kupata na kufasiri taarifa hizo, na namna ya kufanya maamuzi sahihi katika shughuli za kilimo, sasa ameweza kukabiliana na changamoto ya kutotabirika kwa misimu kunakosababishwa na athari za mabadiliko ya tabianchi.



# WAKULIMA TARIME WANUFAIKA NA MAFUNZO YA UDHIBITI WA MAGONJWA KWA MAZAO NA MIFUGO

**Na. John Qambaro**

Katika jitihada za kuongeza uzalishaji na kupunguza hasara kwa wakulima, Kituo cha kilimo Mogabiri imefanya mafunzo ya udhibiti wa magonjwa kwa mazao na mifugo kwa mafanikio makubwa katika vijiji mbalimbali wilayani Tarime. Mafunzo hayo yaliendeshwa kwa kushirikiana na wataalam wa kilimo na mifugo kutoka Halmashauri ya Wilaya ya Tarime, yakilenga kuwajengea uwezo wakulima kutumia mbinu bora za asili na za kisasa katika kukabiliana na changamoto kwenye mazao na mifugo yao.

Mbinu za asili kama vile matumizi ya mimea tiba kama mwarobaini, pilipili kichaa, na majivu zimefundishwa na kuthibitishwa kuwa na ufanisi katika kudhibiti wadudu waharibifu na magonjwa ya mimea. Kwa upande wa mifugo, wakulima walijifunza mbinu za utunzaji bora, usafi wa mazizi, pamoja na matumizi sahihi ya dawa na chanjo kwa mifugo.

Mafanikio ya mafunzo haya yameonekana ndani ya miezi michache kupitia ongezeko la mavuno, kupungua kwa vifo vya mifugo, na kuongezeka kwa uelewa wa wakulima kuhusu umuhimu wa afya ya mimea na mifugo. Pia, wakulima wameanzisha vikundi vya kubadilishana ujuzi na kutoa msaada wa haraka kwa wenzao pindi matatizo yanapojitokeza. Kupitia mafunzo haya, jamii ya wakulima Tarime inazidi kuimarika kiuchumi na kijamii, huku ikijenga msingi wa kilimo hai na endelevu.



*Mmoja wa wakulima walioshiriki, Bw. Chacha kutoka kijiji cha Kitenga, alisema, "Tulikuwa tunapata hasara sana kwa sababu ya magonjwa ya mahindi na kuku. Lakini baada ya mafunzo haya, sasa tunajua namna ya kutambua mapema dalili na kutumia tiba za kienyeji pamoja na ushauri wa wataalam"*

### ...KUTANA NA DENIS

Kwa sasa, Denis anatumia taarifa za hali ya hewa na tabianchi kufanya maamuzi sahihi katika kilimo, hususan kutambua lini msimu unaanza, kiasi cha mvua katika msimu husika, na ushauri juu ya aina ya mazao yanayopaswa kupandwa katika msimu huo. Kwa sasa, Denis alisema kuwa anaweza kupata taarifa hizo kupitia redio, magazeti, na kutoka kwa maafisa ugani kupitia mikutano ya kijiji ambao hupata taarifa hizo moja kwa moja kutoka tovuti za mamlaka husika kama Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA).

Kupitia taarifa hizo, ameweza kufanya maamuzi mbalimbali (hasa katika msimu uliopita). Aliweza kutambua msimu kwa usahihi (mvua zilianza wiki ya pili ya mwezi Machi), akaandaa shamba mapema, na pia aliweza kuchagua mbegu za muda mfupi (mahindi) kwa kuwa utabiri ulionyesha mvua zitakuwa za wastani.

Baada ya kutumia taarifa hizo na kufanya maamuzi hayo, ameona manufaa makubwa — mazao yalikuwa mazuri, aliweza kupata mavuno ya kutosha, akahifadhi kwa ajili ya chakula na kuuza sehemu ya mazao kwa kuwa soko lilikuwa zuri, hivyo akapata kipato.

Yote hayo yasingewezekana bila kupokea mafunzo kutoka Kituo cha Maendeleo ya Kilimo cha Mogabiri na kutumia mafunzo hayo kwa ufanisi. Denis alisema: "Napenda kushauri jamii yangu na jamii nyingine nyingi zinazotegemea kilimo katika maisha yao ya kila siku kuwa ni vyema kutumia taarifa za hali ya hewa na tabianchi katika shughuli zao za kilimo. Watakuwa na uwezo wa kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi katika maisha yao na kunufaika kwa njia mbalimbali, hasa kuendelea kukuza uchumi wao na kupambana na umaskini katika maisha yao.

Kupitia simulizi hii ya Denis, tunajifunza kuwa katika kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi katika jamii zetu, matumizi ya taarifa za hali ya hewa ni suluhisho kwa wakulima wadogo, ili kuendelea kuboresha maisha yao hasa katika shughuli zao za kilimo na ufugaji.

# KITUO CHA KILIMO MOGABIRI, YASAIDIA SHULE KUBORESHA LISHE NA AFYA KWA WATOTO.



**Na. John Qambaro**

Kituo cha Kilimo cha Mogabiri, kimeendelea kuonyesha moyo wa kutoa huduma kwa jamii kwa kusaidia shule za msingi za Kitenga, Turugeti na Kwisarara katika utekelezaji wa mradi wa lishe kwa wanafunzi. Kupitia mradi wa usalama wa chakula, MFEC imetoa msaada wa vyombo muhimu vya kupikia na kula ikiwa ni pamoja na Vikombe, Sahani, na Sufuria kubwa kwa ajili ya maandalizi ya chakula shuleni.

Mbali na vifaa hivyo, kituo pia kimewezesha ujenzi wa mifumo ya kuvuna maji ya mvua katika shule hizo ili kuwezesha upatikanaji wa maji safi kwa matumizi ya jikoni na usafi wa mazingira. Hatua hii imekuja wakati ambapo shule nyingi za vijijini hukabiliwa na changamoto ya maji, hali inayozorotesha jitihada za kuboresha lishe ya wanafunzi.

*Bw. Lucas Teddy, Mwalimu kutoka Shule ya Msingi Turugeti, anasema: "Msaada huu umetusaidia sana. Sasa wanafunzi wanapata uji na chakula cha mchana shuleni kila siku, na tuna uhakika wa maji kwa matumizi ya kupikia na usafi."*



Kupitia mradi huu wa lishe shuleni, wanafunzi wanapata mlo wa pamoja wenye virutubisho, hali inayochangia kupunguza utoro, kuongeza umakini darasani, na kuboresha afya zao kwa ujumla. Viongozi wa jamii na wazazi pia wamekuwa wakihamasishwa kushiriki katika maandalizi ya chakula na utoaji wa chakula shuleni.

Kwa msaada huu, Mogabiri Farm Extension Centre inaendelea kuimarisha mchango wake katika kuinua ustawi wa watoto na kuunga mkono maendeleo ya elimu na afya vijijini.

## SHUGHULI ZINGINE KATIKA PICHA



Picha: Mafunzo VICOBA



Picha: Mafunzo ya Uvunaji Bora



Picha: Mpango wa Lishe



Picha: Upandaji wa Miti



Picha: Uvugaji wa Kuku

# SAFARI YA NUHU KERARYO KATIKA MATUMIZI YA TAARIFA ZA HALI YA HEWA.



Bw. Nuhu Keraryo, mwenye umri wa miaka 54, ni mkulima aliyejitolea katika kijiji cha Kewamamba na ameona mabadiliko ya ajabu katika mazoea yake ya kilimo kutokana na mtazamo wake makini wa kupata na kutumia taarifa za hali ya hewa. Kwa miaka mingi, Nuhu alikabiliwa na changamoto mbalimbali katika shughuli zake za kilimo, ikiwa ni pamoja na mvua zisizo na uhakika na mavuno machache ya mazao yanayotokana na kilimo holela. Walakini, mabadiliko yalitokea wakati alianza kutumia nguvu ya habari ya hali ya hewa.

Kwa miaka mingi, Nuhu, kama wengi huko Kewamaba, alitegemea tajriba ya kibinafsi na makadirio ili kuongoza ratiba zake za upandaji na upanzi. Matokeo yake mara nyingi yalikuwa ya kukatisha tamaa mavuno kutokana na mbegu kuoza mashambani wakati mvua haikufika kwa wakati. Mabadiliko ya hali ya hewa yalizidisha changamoto hizi, na kuleta mifumo isiyotabirika ya hali ya hewa na hali mbaya zaidi.

Safari ya Nuhu kuelekea mabadiliko ilianza aliposhiriki mafunzo yaliyosimamiwa na Kituo Kilimo Mogabiri na maafisa ugani. Wakati wa mikusanyiko hii ya taarifa, alijifunza kuhusu umuhimu wa taarifa za hali ya hewa na uwezekano wake wa kuleta mapinduzi katika ukulima wake. Nuhu aligundua kuwa utabiri wa hali ya hewa unaweza kumsaidia kufanya maamuzi sahihi kuhusu wakati wa kupanda, aina gani ya mazao ya kuchagua, na jinsi ya kujiandaa kwa changamoto zinazoweza kutokea kama vile magonjwa.

Akiwa na ujuzi huu mpya, Nuhu aliamua kuchukua mtazamo wa makini kwa shughuli zake za kilimo. Alipata taarifa za hali ya hewa zilizoonyesha mvua kubwa katika ukanda wa Ziwa Victoria, hivyo kumwezesha kujipanga vilivyo. Pamoja na familia yake, alichagua kwa uangalifu tarehe mwafaka ya kuanza kupanda, akiipatanisha na msimu wa mvua uliotarajiwa. Uamuzi huu wa kimkakati, ulioshauriwa na wataalamu wa kilimo, ulimsaidia kuepuka kuoza kwa mbegu na vikwazo vingine vinavyohusiana na hali ya hewa.

Safari ya Nuhu haikuishia kwenye mabadiliko yake mwenyewe; alishiriki ujuzi wake na wanajamii kupitia kikundi chake cha Jiendeleze. Alikua mtetezi wa matumizi ya taarifa za hali ya hewa katika kilimo na akawahimiza wakulima wenzake kukumbatia rasilimali hii muhimu.

Matokeo ya juhudi za Nuhu yamekuwa ya ajabu kweli kweli. Mavuno yake yameshuhudia ongezeko kubwa ikilinganishwa na misimu iliyopita ambapo alitegemea kilimo cha mazoea. Kwa kutumia taarifa za hali ya hewa kuongoza maamuzi yake, alipunguza hasara iliyosababishwa na mvua zisizotarajiwa, na hatimaye kusababisha maisha yenye mafanikio na utulivu.

Hadithi ya Nuhu Keraryo ni mfano angavu wa jinsi upatikanaji na utumiaji wa taarifa za hali ya hewa unaweza kuwawezesha wakulima kufanya maamuzi sahihi, kuboresha mavuno yao kwa kiasi kikubwa, na hatimaye kuboresha maisha yao. Anaendelea kujitolea kutumia taarifa za hali ya hewa ili kufahamisha maamuzi yake ya baadaye ya kilimo na kuendelea kuwaelimisha na kuwatia moyo wanajamii wenzake kufanya vivyo hivyo.


**Mogabiri Farm Extension Centre**

**P.O.Box 134,**
**Tarime-Mara**
**Phone: 0784530 506**
**0685232 056**
**E-mail: manager.mfec@gmail.com**